

## Mbegu na Matunda ya Udugu

Maazimio ya mwisho ya Kongamano la Kuadhimisha Miaka 30 ya Udugu KPS – Ukanda wa Kusini 28 Septemba – 1 Oktoba 2006 mjini Njombe, Tanzania

1. Tunatambua kwa shukrani kwamba kwa mara ya kwanza wajumbe wa dayosisi zote na majimbo (Propsteien) yote ya KPS kutoka ngazi zote wakiwemo wajumbe viongozi pamoja na washarika walihudhuria katika kongamano hili.
2. Mkutano huu wa wajumbe wa uongozi pamoja na washarika ulikuwa na umuhimu mkubwa kwetu. Liliibuka swali jinsi ya kuendeleza uhusiano huo siku za usoni pia.
3. Kongamano linapendekeza kurudia mkutano kama huo (labda wenye idadi ndogo zaidi ya wajumbe) kila baada ya muda fulani, kwa mfano kila baada ya miaka mitano. Pendekezo jingine ni kuanzisha kamati za udugu kwenye makontinenti mawili zilizo na wajumbe wa ngazi zote mbili. Matokeo yake yajulishwe kwa ndugu ng'ambo.
4. Tunatambua kwamba uwazi ni kipengele muhimu katika kuendeleza udugu wetu. Maana ya uwazi ni kuwajulisha ndugu pamoja na ngazi nyingine husika kuhusu kiwango na lengo la misaada. Pia maana ya uwazi ni kuweka wazi uhusiano na ndugu wengine. Uwazi unasaidia kuzuia rushwa na kutumia vibaya fedha na rasilimali.
5. Siku za usoni tusiruhusu miradi na fedha zitawale udugu wetu. Msingi wa udugu wetu ni kwamba sisi kama Wakristo tunahitajiana katika njia yetu ya kwenda kwa Bwana wetu katika kutafuta ufalme wa Mungu. Katika historia ya udugu wetu na pia siku za usoni hilo linadhihirika hasa katika kuombeana (kwa mfano Jumapili ya Rogate).
6. Katika matendo yetu yote tukumbuke kwamba Yesu alituita kuwa taifa lake, na maana yake ni kanisa moja miongoni mwa watu maskini na kwa ajili ya maskini. Kanisa lisiache nyuma watu maskini.
7. Sehemu ya umoja katika udugu ni kwamba wanaume na wanawake wanashiriki sawa katika ngazi zote za uwajibikaji.
8. Kutokana na masomo ya Biblia wakati wa kongamano tulipata maarifa jinsi ilivyo muhimu na jinsi inavyozaa matunda ikiwa tunasoma Biblia pamoja tukizingatia miktadha tofauti. Ni masomo ya Biblia yanayozingatia tamaduni tofauti.
9. Tunapendekeza kwamba masomo ya pamoja ya Biblia yawe kipengele cha kudumu cha udugu wetu. Kwa mfano wakati wa safari na matenbezi ya udugu uwekwe muda maalum kwa masomo ya Biblia ya aina hiyo yanayozingatia tamaduni tofauti. Pamoja na hayo tunasisitiza kwamba kutembeleana na kubadilishana vijana wanaojitolea na watumishi ni muhimu.
10. Tunatambua kwamba makanisa katika nchi zote mbili si nguvu kuu tena inayoongoza katika masuala ya maisha, dini na maadili. Kwa hiyo tunapendekeza kuwasomesha wachungaji wetu (pamoja na wachungaji wanawake) vizuri kwenye kiwango cha juu katika udugu wetu ili tuweze kutoa mchango unaohitajika katika jamii yetu siku za usoni.

11. Tunatambua kwamba udugu wetu ulikua vizuri pale ambapo ilisisitizwa kujifunza lugha. Kwa hiyo tunapendekeza kwa siku za usoni kuboresha ujuzi wa Kiswahili na Kijerumani.
12. Wakati uliopita KPS ilikuwa na nguvu ya kuanzisha uhusiano wa udugu uliozaa matunda na miradi katika ngazi mbalimbali. Kwa hiyo tunatumaini kwamba mtandao uliopo wa uhusiano uenezwe siku za usoni. Hasa uhusiano kati ya sharika na uongozi ulijitokeza kuwa muundo uliozaa matunda. Uhusiano huo usitoweke wakati wa kuunganisha KPS na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Thuringia.
13. Tunashukuru kwamba historia ilileta mabadiliko katika ufahamu na matendo ya misioni. Sasa sisi ni ndugu katika misioni. Tunahitajiana kwa sababu ni kweli kwamba tunaweza kuishi na kushuhudia imani kwa pamoja tu.
14. Tunaona ni muhimu kuanzisha kamati ya udugu kwa dayosisi zote sita za Ukanda wa Kusini wa Tanzania.
15. Mwishoni tunasisitiza kwamba udugu wetu ni zawadi kutoka kwa Mungu. Zawadi hiyo haikustawi na haitastawi bila baraka ya Mungu.